

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA HAMSINI**

**20 JUNI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI TAREHE 20 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

642. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI  
(LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Wazee wanaostaafu watapata Mafao yao  
kwa wakati.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**643. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itarekebisha mipaka ya Vijiji vya Kata ya Utengule na Usongwe ikiwemo Kijiji cha Mbalizi ambacho hakiungani kabisa na Vijiji vingine.

**644. MHESHIMIWA ALLY YAHAYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itanunua Magari ya Wagonjwa kwa ajili ya Vituo vya Afya vya Nanyumbu, Michiga na Mtambaswala.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**645. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga ili kurahisisha mawasiliano.

#### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

##### **646. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wananchi wanaochukua mafuta baada ya magari ya kubeba mafuta kupata ajali.

#### **WIZARA YA UJENZI:**

##### **647. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakabidhi majengo yaliyotumiwa na Mshauri wa Ujenzi wa Barabara ya Mbinga hadi Mbambabay kwa Halmashauri ya Nyasa.

**648. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Karatu – Mang’ola - Matala hadi Lalago kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA KILIMO:**

**649. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje kuwahusisha Vijana waliomaliza mafunzo ya JKT waliopo katika Vikosi na waliohitimu katika mpango wa *Block Farming*.

**650. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLAH AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni kwa kiwango gani TEHAMA inatumika kuboresha Sekta ya Kilimo nchini.

#### **IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024  
*(The Finance Bill, 2024).*

#### **V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
20 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**